KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

GRADE 8 — END OF TERM 2 EXAMINATION 2026

KISWAHILI: LUGHA

Karatasi ya 1

KJSEA 902/1

TIME: Saa 1 dakika 40

Candidate's Name		**Adm Number**	
School Name		**School Code**	
Candidate's Signature		**Date**	

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Karatasi hii ina maswali 50 ya kuchagua jibu.

2. Jibu maswali YOTE kwenye karatasi ya majibu uliyopewa.

3. Tumia penseli ya kawaida, aina ya HB.

4. Andika majibu yote kwa lugha ya Kiswahili.

SEHEMU A: (Alama 50)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 1 hadi 8.

Ugojwa wa kisukari umekuwa tatizo kubwa sana katika nchi nyingi duniani. Ugonjwa huu husababishwa na hali ya damu kuwa na sukari nyingi kuliko inavyohitajika. Mwili wa binadamu una chombo kidogo kinachojulikana kama kongosho, ambacho huzalisha kemikali inayoitwa insulini. Insulini husaidia seli za mwili kupokea sukari kutoka damu na kuitumia kama chanzo cha nguvu. Iwapo kongosho haifanyi kazi vizuri, sukari hukusanyika damu, na hii ndiyo husababisha
kisukari.

Kuna aina kuu mbili za kisukari. Aina ya kwanza huathiri watu tangu utotoni, na mara nyingi haihusiani na tabia ya mtu. Aina ya pili, ambayo ni ya kawaida zaidi, husababishwa na mambo kama vile unene kupita kiasi, kutotumia mwili ipasavyo, na kula vyakula vilivyo na sukari nyingi.
Ugonjwa huu unaweza kudhibitiwa kwa kupunguza uzito, kufanya mazoezi ya mwili mara kwa mara,
na kula chakula chenye afya.

Dawa za kisukari zinapatikana, lakini haziponyeshi ugonjwa huu kabisa. Watu wengi wanaoishi na kisukari lazima waendelee kuchukua dawa maisha yao yote na kukaguliwa na daktari mara